# Kristo 7



Published by the Comic Bible Society, LLC
Copyright © 2021

Kingstone Comics maintains copyright to this comic book as provided by United States copyright law.

Print and digital copies of this version may be freely distributed without penalty under a Creative Commons license.




MATHAYO 17:22-25, MARKO 9:30-32; LUKA 9:43-45






MATHAYO 17:25-27


YESU ALIKAA ENEO LA GALILAYA KWA SABABU WENGINE YUDEA BADO WALITAKA KUMUUA.
NDIYE YULE.
SHEREHE YA MAKAO, ILIYOSHEREHEKEWA YERUSALEMU ILIKUWA KARIBU NDUGU WAKE YESU WALIPOMPATA.
YESU, NJOO YUDEA WAONE MIUJIZA YAKO!
MSIFANYE VITU KISIRI.
DUNIA HAIWACHUKII, YANICHUKIA MIMI MAANAKE NAONGEA KUHUSU UOVU WAKE.
KWA HIYO NITAENDA MDA UKIWADIA TU.
NDUGU ZAKE WENYEWE HAWAMWAMINI.
YESU ALIKAA GALILAYA KWA MDA HUO, AKIENDELEA KUFUNDISHA NA KUPONYA.
NINAVYOONA PETERO NA ANDREYA NDIO WAKUU KATI YETU.
KISHA MI NA WEWE.
YAANI WAMAANISHA MIMI KISHA WEWE.
LA NIMESEMA NINACHOMAANISHA...
MATHAYO 18:1; MARKO 9:33; LUKA 9:46; YOHANA 7:1-9






MATHAYO 9:2-35, 18:15-17; MARKO 9:33-50; LUKA 9:47-50


HUKO SAMARIA ALITUMA WATU WAMTAYARISHIE MAHALI.
WALIPORUDI...
YESU, HAWAKUTAKI KABISA!
INAFAA TUITE MOTO TOKA MBINGUNI UWAANGAMIZE KWA KUKUKANA WEWE!
WAANGAMIZE?
KWA NINI YAKOBO?
LA! TUTOE VUMBI WAYONI TWENDE KIJIJI CHENGINE.
RABBI! WAENDA WAPI?
NTAKUFUATA KWA VYOVYOTE VILE!
MBWEHA WANA NYUMBA, NDEGE WANA VIOTA LAKINI MWANA WA ADAMU HANA MTO WA KUKIWEKA KICHWA CHAKE.
NIFUATE.
NDIO! LAKINI ACHA NIMZIKE BABANGU.
WACHA WAFU WAJIZIKE; NJOO NAMI USEME JUU YA UHAI UPATIKANAO KWENYE UFALME WA MUNGU!
NTAKUFUATA NIKIWAAGA JAMAA WANGU!
JE WAWEKA MKONO KWENYE JEMBE KISHA KUTAZAMA NYUMA?
LA, WAANGALIA MBELE! HIVYO NDIVYO INAPASWA KUTUMIKIA UFALME WA MUNGU!
KWA HIYO YESU NA WANAFUNZI WAKE WAKAELEKEA YUDEA.
NA YERUSALEMU AMBAKO ALIENDA KWENYE SHEREHE YA MAKAO KWA USIRI.


WATU WENGI TOFAUTI WALIMTAZAMA YESU YERUSALEMU WAKITARAJIA AJE KWENYE SHEREHE.
...NASKIA NI MTU MZURI!
LA, ANAJUA TU KULAGHAI!
KATIKATI YA KUSHEREHEKEA SHEREHE YESU ALIJITAMBULISHA.
WAWEZAJE KUWA NA KISOMO CHA KIWANGO KILE BILA KUSOMA KAMA RABBI WENGINE?
MAFUNZO YANGU SI YANGU!
YATOKA KWA ALIYENITUMA!
UKIFANYA MAPENZI YA MUNGU UTAONA MAFUNDISHO YANGU YANAKOTOKA!
HUYU SIYE YESU WALIYETAKA KUMUUA?
HAWAMWAMBII LOLOTE ANAPOFUNZA!
LABDA SASA WANAFIKIRIA NI KRISTO!
KAMA MNA KIU NJOONI KWANGU MNYWE!
KAMA MNANIAMINI MAJI YA UZIMA YATATIRIRIKA TOKA KWENU!
HUYU JAMAA NI NABII!
LA! YEYE NI KRISTO!
KRISTO HAPASWI KUTOKA GALILAYA!


TULITUMA WALINZI WAMKAMATE HUYU YESU LAKINI WAO PIA WALILAGHAIWA NA MATAMSHI YAKE.
WATU WAMEGAWANYIKA.
AENDELEA KUFUNZA. KILA SILU.
TUTAMKOMESHA VIPI?
SHERIA YETU HAITURUHUSU KULAANI BILA KUELEWA ANACHOKIFANYA.
NIKODEMO, MANABII HAWATOKI GALILAYA!
NINA WAZO...
ASUBUHI ULIOAMKIA.
...ALIYENITUMA NI MKWELI!
HAMUMJUI LAKINI NAMJUA KWA KUWA NDIYE ALIYENITUMA!
MWALIMU!
MWALIMU, MWANAMKE HUYU ALIPATIKANA AKIZINI!
SHERIA YA MUSA YATUAMBIA TUMPIGE MAWE!
WEWE WASEMAJE?
TUFANYEJE MWALIMU?
TWAMBIE!
"ALIYEKUTUMA" ASEMAJE?


NDIO. MPURE MAWE.
NA ACHA ASIYE NA DHAMBI ARUSHE JIWE LA KWANZA.
WATU WAMEENDA WAPI?
KWANI HAKUNA ATAKAYEKULAANI HAPA?
HAKUNA, BWANA.
NAMI SITAKULAANI.
ENDA NA USIFANYE DHAMBI TENA.
ACHA MAISHA YA DHAMBI!
NDIO BWANA! NITAFANYA!


WAKATI MWENGINE YESU ALIAMBIA UMATI...
MIMI NI MWANGA WA DUNIA.
UKINIFUATA HUTATEMBEA GIZANI KAMWE.
BADALA YAKE UTAKUA NA MWANGA WA MAISHA!
USHUHUDA WAKO HAUNA UZANI!
U SHAHIDI MWENYEWE!
USHUHUDA WANGU NI KWELI.
SHERIA YASEMA YAPASWA USHUHUDA WA WATU WAWILI.
NINAO.
MIMI.
NA BABA, ALIYENITUMA
KUBALI!
WEWE NI MSAMARIA!
NA ALIYE PAGAWA IKIZIDI!
LA.
NAMTII BABANGU NA MNAKOSA KUNITII!
IBRAHIM BABU YENU ALISHEREHEKEA ALIVYOFIKIRIA SIKU YANGU KUJA ITAFIKA!
NA ALIIONA!
NA AKAFURAHIA!
HATA HUJAFIKA MIAKA HAMSINI!
LAKINI WADAI KUMUONA IBRAHIM?
NAWAAMBIENI--
--KABLA IBRAHIM KUZALIWA--
NDIMI!


MPIGE MAWE! UZUSHI!
KAMA WEWE NI MYAHUDI MCHA MUNGU --
LAKINI--
--BASI CHUKUA JIWE UMPURE!



YOHANA 8:59


TAFADHALI... SAIDIA ALIYEZALIWA KIPOFU!
MWALIMU, NANI KATI YA MTU HUYU NA WAZAZI WAKE ALIFANYA DHAMBI?
ADHABU HAIKOSI NI YA WAZAZI KAMA ALIZALIWA KIPOFU!
LA.
HAMNA.
HILI LAFANYIKA NDIO NGUVU ZA MUNGU ZIDHIHIRIKE NDANI YAKE.
TWAFAA TUFANYE KAZI YA ALIYENITUMA KUNGALI MCHANA.
USIKU UKIJA HAKUNA ATAKAYEFANYA KAZI.
NINGALI DUNIANI NI MWANGA WA DUNIA.
PTOOOO
NANI HUYO?
ENDA.
OGA KWENYE KIDIMBWI CHA SILOAMU.
NI...NI....
BAADAYE KIPOFU ALIFANYA ALIVYOSEMA YESU--
ALIONGEA KWA MAMLAKA. NI NANI?
NIMESIKIA ANAITWA YESU.

YOHANA 9:1-7


--ALIULIZWA MASWALI NA MAFARISAYO.
HAWAKUPENDA MAJIBU YAKE.
HUYU LAZIMA ATOKA KWA MUNGU!
ALINIPONYAJE!
MBONA WATUPA MSOMO?
UMEKUA KATIKA DHAMBI TANGU KUZALIWA!
JAMBO!
WAMWAMINI MWANA WA ADAM?
NILIPONYWA NA MTU.
WAJUA NI NANI?
NIAMBIE NI NANI NIMWAMINI!
WAMUONA SASA HIVI!
BWANA!
NAAMINI!
NIMEKUJA VIPOFU WAONE NA WANAOONA WATAGEUKA VIPOFU.
NINI?
TU VIPOFU?
MNGEKUA VIPOFU HAMNGEKUWA WENYE DHAMBI.
LAKINI KUJIDAI MWAONA, MNA HATIA.
MIMI NI MCHUNGAJI BORA ANAYETOA MAISHA YAKE KWA KONDOO WAKE.
KIBARUA HUKIMBIA AONAPO MBWA MWITU AKIJA.
HAJALI JUU YA KONDOO.


KAMA MCHUNGAJI MZURI NAJUA KONDOO WANGU.
NA KONDOO WANGU WANIJUA!
NA NAWATOELEA KONDOO WANGU MAISHA YANGU!
HAKUNA AYACHUKUAYE. NAYATOA MWENYEWE.
NINA MAMLAKA YA KUYATOA.
NA MAMLAKA YA KUYACHUKUA TENA.
YATOKA KWA BABA YANGU.
ANA KICHAA!
AMEPAGAWA! MBONA MTU AMSIKIZE?
PEPO AWEZA KUPONYA MACHO YA KIPOFU?
WAKATI HUO YESU ALIWAZUNGUMZIA WAFUASI SABINI NA WAWILI AKIWAPA KAZI:
ENDENI!
NAWATUMA KAMA NJIWA MIONGONI MWA MBWA MWITU!
MKIENDA KWENYE MJI NA KUKARIBISHWA KULENI MNACHOPEWA.
PONYA WAGONJWA NA MUWAHUBIRIE KUWA UFALME WA MUNGU U KARIBU.
MSIPOKARIBISHWA ENDENI NJIANI MKIFUTA VUMBI KUTOKA KWA VIATU VYENU--



ANAYEWASIKIZA ANISKIZA MIMI!
ANAYEWAKANA ANIKANA MIMI!
NA ANAYENIKANA AMKANA ALIYENITUMA!
WALIPORUDI...
ILIKUWA AJABU YESU!
HATA MAPEPO WALINYENYEKEA KWA JINA LAKO!
RAFIKI ZANGU, NILIMUONA SHETANI AKIANGUKA KAMA UMEME TOKA MBINGUNI.
NILIWAPA MAMLAKA KUMSHINDA ADUI!
LAKINI FURAHI, BADALA YAKE, KWA KUWA MAJINA YENU KAANDIKWA MBINGUNI!
BABA, NAKUTUKUZA SABABA WAFICHA MAMBO HAYA KUTOKA KWA WENYE HEKIMA NA WALIOSOMA--
--NA KUMUONYESHA MTOTO!
BABA TU NDIYE AMJUAYE MWANA.
NA AMJUAYE BABA NI MWANA--
NA ANAYEMCHAGUA KUMUONYESHA MWANA.
BAADAYE ALIVYOONGEA NA WALE THENASHARA PEKE YAKE YESU ALISEMA:
HERI MAISHA YENU!
KWA KUWA MANABII NA WAFALME WALITAMANI KUONA NA KUSIKIA MNACHO.
LAKINI HAWAKUONA!




LUKA 10:12-24


SIKU MOJA MTAALAM WA SHERIA ALITAKA KUMJARIBU YESU:
RABI, SWALI!
NIFANYEJE KUUPATA UHAI WA MILELE?
SHERIA YA MUSA YASEMAJE?
“MPENDE BWANA MUNGU WAKO NA MOYO, ROHO, NGUVU NA NIA."
NDIO.
NA "MPENDE JIRANI YAKO KAMA UNAVYOJIPENDA MWENYEWE."
NDIO! FANYA HIVYO UTAISHI!
LAKINI JIRANI YANGU NI NANI?
ACHA NIWAPE HADITHI.
MSAFIRI ALISHAMBULIWA NA KUIBIWA--
--NA KUACHWA AFE.
KUHANI ALIPITA NA KUMPITA.
MSAIDIZI WA HEKALUNI AKAFANYA VIVYO HIVYO.
LAKINI MSAMARIA ALIMUONA AKAMHURUMIA.
ALIMSAIDIA KUMPELEKA MAHALI SALAMA NA KULIPIA HUDUMA YAKE.
KWA HIYO JIRANI NI NANI?
ALIYEMHURUMIA.
KABISA.
HAYA, ENDENI SASA MFANYE VIVYO HIVYO
LUKA 10:25-37


NJE YA BETHANIA, MJI ULIOKARIBIA YERUSALEMU.
YESU! HUJAMBO!
YESU, WEWE NA WANAFUNZI WAKO TAFADHALI PUMZIKENI NA MKE KWANGU!
KAKANGU LAZARO DADANGU MARIA NAMI TUTAFURAHI!
TUNGEJAWA NA FURAHA!
SALAMA, YESU!
KARIBU! ASANTE KWA KUUKUBALI MWALIKO WA MARTA!
KUNA CHOCHOTE KINGINE UNGEPENDA KABLA SIJALETA CHAKULA?
LA MARTA ASANTE.
MARIA WAWEZA KUNISAIDIA.
NDIO. DAKIKA MOJA.



LUKA 10:38-39


"DAKIKA MOJA" BAADAYE...
YU WAPI?
KUNA MENGI YA KUFANYA!
HIYO SI SAWA!
...SI MATENDO YAKO BALI MOYO WAKO...
BWANA!
MWAMBIE MARIA ANISAIDIE!
HUJALI KUA ANIACHA NIFANYE KAZI YOTE PEKE YANGU?
MARTA UNA WASIWASI NA KUKASIRISHWA NA VITU VINGI VIDOGO.
KITU KIMOJA TU UNAFAA KUKIWAZA.
MARIA AKIJUA NA HICHO HAKITACHUKULIWA TOKA KWAKE.

LUKA 10:39-42


SIKU NYENGINE YESU ALIPOENDA KUOMBA.
BWANA WAWEZA KUTUFUNDISHA KUOMBA?
KAMA YOHANA MBATIZAJI ALIVYOWAFUNDISHA WANAFUNZI WAKE?
NDIO.
MNAPOOMBA SEMENI:
BABA YETU.
JINA LAKO LI TAKATIFU.
UFALME WAKO UJE.
TWAKUOMBA CHAKULA TUNACHOHITAJI.
NA TWAKUOMBA UTASEMEHE DHAMBI ZETU--
--TUNAVYO-WASAMEHE WANAOTUKOSEA.
NA USITUACHE TUINGIE KATIKA MAJARIBU.
ULIZA UTAPATA; TAFUTA UTAPATA; BISHA NA MLANGO UTAFUNGULIWA.
MAANAKE MTOTO AKIULIZA SAMAKI BABA AINA GANI HUMPA NYOKA?
AMA AKIULIZIA YAI BABA AINA GANI ATAMPA MWANAE NGE?
KAMA NYINYI NA UOVU WENU MWAJUA KUWAPA ZAWADI NZURI--
--KWA HAKIKA BABA YENU WA MBINGUNI ATAWAPA ROHO MTAKATIFU WALE WANAOMUULIZA!


LUKA 11:1-13


BAADAYE...
YESU! NAJUA UMEPONYA WENGI!
TAFADHALI MPONYE RAFIKI YANGU!
HAWEZI KUSEMA!
AMEPAGAWA!
NDIO MAANA NI BUBU!
SIO KWA MDA MREFU...
NAAMURU PEPO ANAYEMUATHIRI MTU HUYU--
--MUONDOKEE!
A...A...
ASANTE...


NI KUPITIA BEELZEBUB MKUU WA MAPEPO--
--ANA UWEZO WA KUTOA MAPEPO
UFALME AU NYUMBA ILIYOTENGANA ITAANGUKA!
UFALME WA SHETANI UTASIMAMA VIPI KAMA KUNA KUTANGANA MLE NDANI?
NA NIKITOA MAPEPO KWA JINA LA SHETANI--
--BASI WATU WENU WATAWATOA KWA JINA GANI?
FAHAMU: KAMA NA NGUVU ZA MUNGU NITUMIAZO KUWATOA--
--BASI UFALME WA MUNGU U NANYI!
HERI NI MWANAMKE ALIYEKUZAA NA KUKULEA!
WAJUA HERI NANI?
ANAYESIKIA NA KUTII NENO LA MUNGU!
NANI AWASHAYE TAA NA KUIWEKA CHINI YA BAKULI?
HAKUNA! WAIWEKA UTAKAPOUONA MWANGA!
KWA HIYO HAKIKISHA MUMEJAWA NA MWANGA, SIO GIZA!
UKIJAWA NA MWANGA UTANGAA!



LUKA 11:15-35


ALIPOMALIZA KUNENA...
RABI, WAWEZA KUJA KULA NAMI JIONI?
RABI, WAWEZA KUJA KULA NAMI JIONI?
NINA MASWALI MENGI.
NA NAJUA UNA MAJIBU MENGI!
HAUKU... HUKUNAWA MIKONO.
WAWEZAJE KUKOSA KUNAWA MIKONO?
NYINYI MAFARISAYO...
MWAOSHA NJE YA CHOMBO.
LAKINI NDANI MUMEJAWA NA UROHO NA UOVU TELE!
WAPUMBAVU! JE, MUNGU HAKUUMBA MILI NA ROHO ZENU?






LUKA 11:42-12:1


HAKUNA NENO LILILOSITIRIKA AMBALO HAILITAFUNULIWA!
MANONG'ONEZANO GIZANI YATASIKIKA KWENYE MWANGA!
MSIOGOPE WANAOUA MWILI TU!
MWOGOPE YULE AMBAYE BAADA YA MWILI KUFA ANA NGUVU ZA KUWATUPA JEHANAM!
LAKINI MUNGU AWAJALI HATA SHOMORO!
NA NYINYI? YWAJUA MNA NYWELE NGAPI KICHWANI!
KWA HIYO MSIOGOPE MNA THAMANI ZAIDI YA SHOMORO!
NIFAHAMU DUNIANI NA NTAWAFAHAMU MBINGUNI!
NIKATAE ARDHINI NA NITAKUKATAA MBELE YA MALAIKA!
HATA HIVYO, ANAYESEMA NENO DHIDI YANGU ATASEMEHEWA.
LAKINI ANAYEKUFURU ROHO MTAKATIFU HATASAMEHEWA.
NA WATAKAPOWAPELEKA KWENYE MASINAGOGI MBELE YA MALIWALI NA WENYE MAMLAKA--
--MSIOGOPE MTAKACHOSEMA!
ROHO MTAKATIFU ATAWAFUNZA CHA KUSEMA!


RABI! MWAMBIE KAKANGU KITU SAWA CHA KUFANYA NIKUGAWA URITHI WAKE NAMI!
MIMI SIO MWAMUZI WENU!
ILA NAWAAMBIENI TAHADHARI DIDHI YA UCHOYO!
MAISHA YENU NI ZAIDI YA KUJILIMBIKIZA VITU!
USIWE NA WASIWASI JUU YA MAISHA YAKO!
UTAKACHOKULA, KUNYWA AU KUVAA!
MAISHA NI ZAIDI YA HIVYO!
YATAFAKARI MAUA JINSI YAMEAVYO! HAYATENDI KAZI WALA KUSOKOTA--
--BALI HATA SULEIMAN NAFAHARI YOTE HAKUVIKWA KAMA YALIVYO?
UTAFUTENI UFALME WA MUNGU NA YOTE MTAONGEZEWA!
HAZINA YENU I WAPI? HAPO NDIPO MIOYO YENU IPO.
UKIONA WINGU LIKITOKA MAGHARIBI WAJUA KUTANYESHA.
UPEPO UKITOKA KUSINI WAJUA KUTAKUWA NA JOTO.
MWAWEZA KUTAFSIRI ANGA LAKINI SIO NYAKATI HIZI!
NDIO! NYAKATI ZA KUTISHA!
PILATO ALIAMRISHA WASUMBUFU HUKO GALILAYA WAULIWE, AKACHANGANYA DAMU YAO NA KAFARA ZA PASAKA!
LAZIMA WALE WAGALILAYA WAMEONA WENYE DHAMBI WA KUTISHIA KUUFIKA MWISHO KAMA HUO!
LA!
DHAMBI NI DHAMBI! MSIPOTUBU NYOTE MTAANGAMIA!

# HADITHI YA MTU ALIYEZALIWA KIPOFU

## "JARIBIO" YOHANA 9:1-41





"NIKAGUNDUA WALIKUWA WAONGEA JUU YANGU."
RABI, ALIYEKOSA NI NANI?
NI NANI ALIYESABABISHA KUPOFUKA KWA MTU HUYU. NI YEYE AMA WAAZI WAKE WALIKOSEA?
"NILIKUWA NIMESIKIA SWALI HILO MBELENI."
NA NI SWALI ZURI!
TALMUS INAVYOSEMA, "ANADHIBU MAKOSA YA BABA HADI KIZAZI CHA TATU NA NNE!"
NAAMINI MTU AWEZA KUKOSEA NDANI YA TUMBO LA MAMAKE MAANA UTAELEZA VIPI--
TOSHA!
HUU SI WAKATI WA BISHANO HILI!
TAFADHALI ENDELEA.
HAKIKA, KWELI.
SAUTI NYENGINE IKAWAJIBU. SAUTI YA UPOLE NA MAMLAKA.
KATI YA MTU HUYU NA WAZAZI WAKE HAKUNA ALIYEKOSEA.
SI DHAMBI ILIYOSABABISHA UPOFU WAKE.
NI KUWA KAZI YA NGUVU ZA BWANA IDHIHIRISHWE SIKU HII!
"NILIMSKIA AKITEMA."
"SIO GENI KWANGU. NIMETEMEWA MATE MARA ZISIOHESABIKA."
"LAKINI HAKUNITEMEA MATE. BADALA YAKE BASI..."
"ALIYAGUSA MACHO YANGU."


"KAYAFINIKA NA MATOPE"
"TUKAONGEA KIDOGO KISHA AKASEMA:"
ENDA SASA.
OGA KATIKA KIDIMBWI CHA SILOAMU.
"BILA SHAKA NILIFANYA ALIVYOSEMA!"
"NA TOPE LILIVYOTOKA MACHONI--"
"--NILIPONA!"



KUCHANGANYA MCHANGA UWE TOPE? SIKU YA SABATO?
BILA SHAKA MTU HUYU HATOKI KWA MUNGU, AMA HANGEPONYA SIKU HIYO!
KAMA MTU HUYU NI MWENYE DHAMBI ANGEFANYAJE JAMBO HILI?
MANABII WASEMA KUPONYWA KWA VIPOFU NI ISHARA YA KUJA KWA MASIHI!
WEWE WASEMAJE?
NI NANI ALIYEKUWA NA MTU HUYU?
SIKUMUONA! BADO NILIKUWA KIPOFU ALIPOYAFINIKA MACHO YANGU!
WAJUA NINI KUMHUSU?
NAJUA NI NABII, ANGALAU.
HAMKUMUONA LAKINI TWAJUA MWASEMA KUHUSU NANI.
ANGEKUPONYA SIKU NYENGINE YOYOTE!
KAMA HAKUWAI KUWA KIPOFU LABDA HUYU YESU ALITULAGHAI!
NINI, MIAKA ISHIRINI ILIYOPITA YESU ALIWAAMBIA WAZAZI WA MTU HUYU WADAI NI KIPOFU?
WAZAZI WAKE WAITWE! TUONE WATASEMAJE!
NGOJA HAPO!
HATUTAKI MUPANGE HADITHI ZENU ZA UONGO!


HUYU NI MWANAO?
NDIO.
NA ALIZALIWA KIPOFU?
NDIO.
NADHANI TWAWEZA KUWACHA MFUMO HUU WA MASWALI.
KILA ANAYEMJUA ASEMA ALIZALIWA KIPOFU.
KAMA ALIZALIWA KIPOFU--
--NI VIPI, JAMANI, SASA AONA?


NAJUA NI MWANANGU.
NAJUA ALIZALIWA KIPOFU.
LAKINI SIJUI ANAVYOWEZA KUONA SASA.
SIJUI ALIYEYAFUNGUA MACHO YAKE.
MUULIZENI YEYE.
ANA UMRI WA KUTOSHA!
AMEHITIMU!
WAONDOE HAPA.
TUTAENDELEA KESHO...
MWANANGU POLE.
WAELEWA, SIO?
KAMA TUNGESEMA HUYU YESU AMEFANYA HIVI BASI...
MAFARISAYO HAWAPENDI WATU WANAOONGEA VIZURI JUU YA HUYU YESU.
NAELEWA.
KWELI.
*"NI KWA KUWA NILIFURAHIA WAKATI WA KWANZA NILIWAONA SIO SIKU HII."*
*"NILIPOWAONA WAKIOGOPA BADILI YA KUNITETEA."*


ULINIREGESHA LAKINI WATAKA KUJUA NINI CHENGINE?
TWATAKA KUJUA NAMNA GANI!
UMEPEWA KIPAWA KIKUU NA WAFAA KUMPA MUNGU UTUKUFU WOTE.
MTU UNAYESEMA ALIKUPONYA NI MWENYE DHAMBI!
KAMA NI MWENYE DHAMBI AU LA NILIKUA KIPOFU SASA NAONA!
KIVIPI?
NIMEWAAMBIA!
KWA NINI MWATAKA KUJUA? MWATAKA KUWA WANAFUNZI WAKE?
WAWEZA KUWA MWANAFUNZI WA MTU YULE LAKINI SISI NI WANAFUNZI WA MUSA!
MUNGU ALIONGEA NA MUSA, TWAJUA HILO KWA HAKIKA!
LAKINI MTU HUYU? HATA HATUJUI ATOKA WAPI!
HATUJUI AMETOKA WAPI?
MWAJUA WATU WANGI WANAOWEZA KUPONYA VIPOFU?
MTU HUYU ATOKA KWA MUNGU, AU HANGEWEZA KUFANYA HIVI!
WEWE NDIO WAONGEA!
ULIZALIWA KIPOFU!
ULIZALIWA KATIKA DHAMBI, MWENYE DHAMBI KABLA HUJAZALIWA!
MUONDOENI HAPA!


SIKU NILIYOJIHISI PWEKE.
KUTUPWA NA WAZAZI WANGU.
KUTUPWA NA WATU AMBAO NILIDHANI WANAFAA KUTUONGOZA KWA MUNGU.
LAKINI SIKUWA PWEKE KWA MDA MREFU.
WAMWAMINI MWANA WA ADAM?
SIKUWAHI KUMUONA MTU ALIYESIMAMA MBELE YANGU.
LAKINI PIA NILIKUWA SIJAPATA MUDA WA KUONA WATU HATA KIDOGO.
KWA NINI? WAJUA JUU YAKE?
NINGEPENDA KUJUA ZAIDI KUMHUSU.
ONA.
WAMUONA SASA.
BWANA WANGU!
NAAMINI!
KWA VITU VYOTE KIPAWA CHA KUONA KIMENIRUHUSU KUONA--
--KUUONA USO WAKE ILIKUWA KITU CHA AJABU KWA VYOTE.

"THE BIBLE EXPLAINED
IN EVERY LANGUAGE."













SUPERBIBLE.TV